**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)**

**MKATABA WA UFUNDI UMEME**
**JENGO LA"SEMI-DETACHED HOUSE"**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 14 mwezi 01 2022

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha Mkoa wa Lindi, S.L.P. 1001, Lindi ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 802 Dodoma (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

SALUM SAIDI LIKWATA S.L.P. 1070, LINDI
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mafia;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya Mafia;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya Umeme hatua ya awali na hatua ya Umaliziaji

**NA KWA KUWA** Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **GHARAMA YA UFUNDI**
   Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 1,528,116.6/=, sema; Shilingi Milioni Moja laki tano Ishirini na nane elfu Mia Moja kumi na Sita na Senti Sita
   Fundi atafanya kazi ya Umeme hatua ya awali na Umaliziaji kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.